Fikranet Connect—Vol 1

# fanikisha NDOTO YAKO

Fahamu uhusiano mkubwa uliopo kati ya Ndoto na Malengo, Vyanzo vya ndoto na Mbinu za Kushughulikia Ndoto zako



Dickson John

YALIYOMO


| | | |
|---|---|---|
| | Shukrani……………………………………. | i |
| 1 | Utangulizi ………………………………….. | 4 |
| 2 | Ishi Ukiwa Ndoto Zako …………………… | 8 |
| 3 | Vyanzo vya Ndoto………………………… | 11 |
| 4 | Vitu vinavyoweza kuipoteza ndoto ………… | 20 |
| 5 | Namna ya kuilinda ndoto yako………..…… | 24 |
| 6 | Fikra pevu iletayo mafanikio ………………. | 28 |
| 7 | jinsi kuwa na fikra chanya ………………….. | 36 |
| 8 | Namna ya kufundisha akili ………………… | 41 |
| 9 | Maumivu ya kuifanikisha ndoto……………. | 48 |
| 10 | Unaanzia wapi – nguvu ya uthubutu ……….. | 67 |
| 11 | Changamoto na vipangamizi katika ndoto na malengo yako ……………… | 79 |

# SHUKRANI

Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye amenijalia heri hadi kufika kuandika kitabu hiki, ingawaje haikuwa kazi rahisi lakini yeyey kanisimamia hadi kuandika utimilifu wote wa kitabu hiki.

Namshukuru mama yangu mpenzio ambaye kwa dua na sala zake nimeweza kukamilisha uandishi wa kitabu changu cha pili baada ya kiwanda mkononi.

Nawashukuru watu kutoka Peace stationery, wachapaji wa kitabu hiki ambao wamenipa ruksa kutumia vifaa vyao hadi kumaliza uandishi wa kitabu hiki. Mwenyezi Mungu mwingi wa heri awajalie Baraka na kuzidi kusonga mbele.

Namshukuru rafiki yangu Darius ambaye amekuwa mchango mkubwa katika kuhariri, maneno ya kitabu hiki mwenyezi Mungu amjalie heri na fanaka katika maisha yake.

# SURA YA KWANZA
# -UTANGULIZI-

***"Huu ni wakati wa kujifunza sio wakati wa kuiga"-***

**N**doto zipo za aina mbalimbali, nyingine zikuwa zinahusishwa na maswala ya imani (dini) nyingine maswala ya sayansi, kadhalika pia nyingine saikolojia ya binadamu. Ndoto ambayo tunakwenda kuizungumzia sio ndoto unayoota ukiwa umelala ni ndoto ya mchana. Ni kile kitu unachotamani kuja kukipata siku moja kabla hujaondoka duniani Ndoto inaweza kua katika makundi ya aina mbalimbali, unaweza kua na ndoto ya kuwa Rais, Mwimbaji bora, Mchezaji bora, Mwandishi Bora, Mfanyabiashara maarufu.

Vile vile unaweza kuwa na ndoto ya kumiliki vitu, nyumba nzuri ya kifahari sana labda ya milioni 300, Gari la kifahari sana, unaweza kuwa na ndoto ya kumiliki utajiri au kuwa Bilionea, Kutembelea nchi fulani na kadhalika. Zote hizo ni ndoto ambazo kila mmoja alikua nazo huenda ni kipindi anakua au hata sasa bado anayo. Kwa bahati mbaya sana watu wengi wamekuwa na ndoto kubwa sana wakiwa wadogo na kuzipoteza walipoanza kuingia kwenye uhalisia wa maisha.

Je, umewahi kusikia hotuba ya moja ya watu maarufu duniani iitwayo ***"I have a dream……….." (nina ndoto)***. Ni miongoni mwa hotuba iliyowahi kushika hatamu na kuwafanya wengi kuwa na morali ya kupigania ndoto zao. Katika maisha lazima kila mtu awe na kitu anachokihitaji katika maisha ili akifanikishe ndipo furaha yake iwe timilifu. Dr. Martin Luther King alikuwa na ndoto ya watu weusi kuishi sawia na watu weupe nchini marekani, ingawa katika mapambano ya kuleta usawa yalikgubikwa na majonzi ya kupotelewa na watu muhimu kama vile Luther King, Watu weusi (Afro-Americans) walifanikiwa kupata haki katika nchi ya marekani. Lengo si kukupa historia ya watu weusi nchini marekani, bali nachojaribu kugusia ni kichwa cha hotuba cha **'*I have a dream".***

Ni lazima kila mtu awe na kitu anachokilenga katika maisha yaani ndoto ili aweze kuishi kwa nidhamu katika ulimwengu huu wa sasa. Kukosa

kuwa na ndoto ni sawa na gari bila mafuta, na kuwa na Ndoto bila Mungu ni sawa na gari bila injini. Hebu fikiria upo kwenye ndege angani halafu hamuna rubani wala muongozaji wa ndege, nini kitakachotokea pindi utakapotaka kutua mahali unapotaka kwenda? Vipi itakapokosa mwelekeo au kuishiwa mafuta/ bila shaka jibu unalifahamu.

Hebu hilo jibu lako liweke kwenye maisha yako yasiyo kuwa na ndoto, ambapo ndoto itapaswa kuwa Rubani au mwongozaji wa ndege na ndege ndiyo iwe maisha yako. Watu wengi hawajui kuwa ndoto zao zina nguvu kubwa kufanikisha maisha yao kijamii, kiuchumi, kisiasa na kila nyanja. Ndani ya ndoto zako kuna kila kitu unachokitaka ama unachokihitaji – iwe fedha, utajiri, umaarufu, familia nzuri, mume mzuri, mke mzuri, watoto wazuri, kazi nzuri, afya nzuri – hivyo ukiacha kutafuta fedha ukatafuta kutimiza ndoto zako utapata kila kitu ikiwemo utoshelevu na amani ya moyo. “***Dream as if you’ll live forever. Live as if you’ll die today” (Kuwa na ndoto kana kwamba utaishi milele. Ishi kana kwamba utakufa Leo) – James Dean***

Mtu pasipo maono, hukosa kujizuia. Na kamwe usipojua unapokwenda hata ukioneshwa njia huwezi kufika. Ndoto ni ramani na mwelekeo wa maisha yako. Hata Mungu mwenyewe anatazamia kuona watu aliwaumba kwa mfano wake wakiwa na kitu wanachotamani kukifanikisha, ndoto ni sawa na maandalio ya moyo ambayo jawabu lake ni Mungu mwenyewe.

Hatuwezi kumuachia Mungu kazi ya kupanga maisha yetu na kuyafanikisha ni kazi ambayo hautaifurahia. Ndio maana mahali Fulani husema leta hoja zako zenye uzito, eleza mambo yako upate kupewa haki yako. Ukikosa ndoto, utakosa maadili binafsi hutojizuia, hutoshughulika kwa namna yoyote, na hata ukipata pesa utakosa cha kufanyia, utaishia kuponda raha na kutumia kwa mambo ya anasa ambayo hayana faida katika maisha yako. Ndoto ni dira yangu ni dira

inayonipa mwelekeo na kunisukuma kuitimiza ili nipate pumziko na furaha ya ndani. **K**ila mtu duniani ana ndoto ingawa haijalishi ni ndoto gani uliyonayo. Ndoto uliyonayo ina thamani kubwa kuliko fedha wala kitu chochote kile. Ndoto uliyonayo ina nguvu kubwa ya kubadilisha maisha yako na kukufikisha sehemu ambayo ulitaka ufike ama zaidi ya pale ulipotarajia kufika.

**N**doto yako ndiyo imebeba kusudi la maisha yako. Kama hutaishi katika ndoto yako maana yake utakuwa hujaishi maisha yako ambayo kwa kiasi kikubwa yapo kwenye ndoto zako. Mtu mmoja aliwahi kusema kuwa, ***watu wengi duniani hawaishi***, ***bali wapo tu.*** Kuna tofauti kati ya kuishi na kuwepo. ***Kuishi*** ni kutimiza ndoto zako na ndani ya kusudi la maisha yako, lakini kama hutimizi ndoto hizo uko nje ya kusudi la maisha yako.

Wewe utakuwa hauishi bali upo upo tu. Anaamka asubuhi kwa sababu watu wanaamka. Ukimuuliza kwanini umeamka anasema ni kwa sababu watu wameamka! Hana sababu za msingi. Kataa kuishi bila agenda, bila kuwa na ndoto ambayo kila siku unapiga hatua kuifikia ama uko ndani yake sasa katika kuitimiza na kuifanikisha kwa kiwango cha juu. Kila kitu kipo kwenye ndoto zako, tafuta kutimiza ndoto zako kuliko kutafuta fedha kwa sababu fedha ni moja kati ya bidhaa iliyomo ndani ya ndoto zako. Sisemi watu wasitafute fedha, la hasha.

Wazitafute, tena kwa bidii, ila wasisahau kutafuta kutimiza ndoto zao na kutumia fedha kama moja kati ya nyenzo za kuwawezesha kutimiza ndoto zao. Ukweli ni kwamba, fedha daima huwa hazitoshi, hata kama ni nyingi kiasi gani. Kama unabisha waulize matajiri kama wamewahi kuridhika. Lakini katika kutimiza ndoto zako kuna utoshelevu kiasi na kuridhika kiasi fulani (satisfaction) hata kama si kwa asilimia 100. Mwandishi mashuhuri wa vitabu, Myles Munroe, aliwahi kusema kuwa

“***Watu wenye kusumbuliwa na msongo mkubwa wa mawazo ni wale ambao ndoto zao hazijtatokea kwenye uhalisia***”

Inawezekana unasumbuka sana kwenye maisha yako kwa sababu hujatimiza ndoto zako, maana ndoto huwa haimwachi mtu akatulia, inampa mahangaiko, mfadhaiko wa kuitafuta. Kila mtu anapaswa azae, ndoto yako izae, uwezo ulionao uzae. Unaweza kukuzalia mafanikio makubwa, hivyo usikubali kufa na kitu cha thamani kilichoko ndani yako. Hakuna ndoto kubwa wala ndogo Fikiria mtu aliyegundua lipstick, leo hii wanawake dunia nzima wanapaka lipstick, si jambo dogo tena. Hukuja duniani kuwa mtu wa kuhangaikia fedha, inatakiwa fedha ikuhangaikie wewe, ikupende na ikutamani na si wewe utamani fedha. . Tengeneza miundo mbinu ya fedha na hiyo miundo mbinu iko kwenye ndoto zako, maono yako, kipaji

KUHUSU MWANDISHI.

Dickson John amezaliwa katika wilaya ya Tarime, kijiji cha Nyamwaga. ni mwandishi wa vitabu mbalimbali vya ujasiriamali na stadi za maisha, na ni mwalimu wa semina mbalimbali katika njia hizi mbili. Amekuwa akifanya kazi hii toka akiwa shule ya sekondari hadi hivi leo. Miongoni mwa vitabu alivyoandika ni pamoja na KIWANDA MKONONI.

KUHUSU KITABU

Kitabu hiki cha Ndoto Yangu – Baraka ya mafanikio, ni kitabu kinachojaribu kugusia kwa upana kuhusu ndoto ambazo wengi tumekuwa nazo lakini wengine hawana. Kinaeleza hatua kwa hatua maana ya ndoto, faida zake na namna ya kuweza kuzifanikisha ndoto zetu haijalishi ni kubwa kiasi gani. Kila ndoto inaweza kutimia tofauti ni muda wa kutimia na namna tunavyozipambania ili kuzitimiza. Changamoto mbalimbali zimeelezwa katika kitabu hiki na namna ya kuzitatua ili kufikia ndoto zako. Je, unatafuta njia rahisi ya kuweka na kutimiza ndoto yako? Kama jibu ni ndio basi kitabu hiki ni kwa ajili yako.